

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: 0262126826  
Nukushi: 026 2126834  
Barua pepe: km@michezo.go.tz  
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali,  
Mtumba, Dodoma  
2 Mtaa wa Habari,  
S. L. P. 25,  
40481 DODOMA.

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUMFUTIA ADHABU BW. ELIAS U. MWANJALA**

**Oktoba 10, 2022 – Dodoma**

Wizara kwa kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) imemsamehe na kumfutia adhabu zote aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mbeya, Bw. Elias U. Mwanjala. Adhabu hizo ni za kutojishughulisha na shughuli za Uongozi wa Michezo kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Disemba 31, 2020 hadi Disemba 31, 2022.

Msamaha huo umetolewa kufuatia ombi lake aliloliwasilisha wizarani la kuomba kusamehewa, ambapo adhabu hiyo ameitumikia kikamilifu kwa zaidi ya asilimia 85.

Aidha, Wizara inapenda kufafanua kuwa wanafamilia wa michezo kote nchini, wanatakiwa kuwa na moyo wa kuvumiliana na kusameheana ili kutumia uwezo na uzoefu wa kila mmoja katika kushauri na kukuza Tasnia ya michezo hapa nchini, kwakuwa Taifa letu bado ni changa na lenye kuhitajiana sote katika kushauri na kuendeleza michezo kwa ujumla.

Pia wadau na familia ya michezo wanasisitizwa kuzingatia na kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa ili kuleta na kuchochea ustawi wa maendeleo ya michezo.

Imetolewa na;

A handwritten signature in blue ink that reads "John Mapepele".

John Mapepele

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**